

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

Telegrams: "MSW"
Telephone: 028 2750271
Fax: 028 2750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz



S.L.P. 170,
MASWA.
SIMIYU.

TAREHE: 17/10/2022

TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE, KUWA HALMASHAURI YA WILAYA INAUZA VIWANJA VILIVYOPIMWA KWA MATUMIZI MBALIMBALI KUPITIA MRADI WAKE WA KUPANGA, KUPIMA NA KUMILIKISHA ARDHI.

VIWANJA HIVYO VINAPATIKANA ENEO LA MALAMPAKA SGR KATIKA KATA YA MALAMPAKA BARABARA INAYOKWENDA SHINYANGA NA MWANZA.

ENEO HILO LA VIWANJA LINAPAKANA NA INAPOJENGWA STESHENI KUBWA YA MIZIGO YA RELI YA MWENDOKASI (SGR) NA BANDARI YA NCHI KAVU (CONTAINER DEPORT). VIWANJA VYOTE VINAFIKIKA KWA BARABARA NA KWAMBA MIUNDOMBINU YA UMEME NA MAJI IPO JIRANI.

MCHANGANUO WA BEI YA VIWANJA VINAVYOUZWA ENEO LA MALAMPAKA SGR NI KAMA IFUATAVYO:-

NA	MATUMIZI YA KIWANJA	BEI YA KILA MITA MOJA YA MRABA TSHS
1	Viwanja vya Makazi	1,300/=
2	Viwanja vya Makazi na Biashara	1,800/=
3	Viwanja vya Biashara	2,800/=
4.	Viwanja vya Hotel site na Nyumba za kulala wageni	2,800/=
5	Viwanja vya kuabudia	2,800/=
6	Lorry Packing	2,800/=
7	Viwanda vidogo na kati (Service Industry) na Maghala (GODWONS)	3,800/=
8	Kituo cha Mafuta	3,800/=

FOMU ZA MAOMBI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA KWA GHARAMA YA TSHS **20,000/=** KWA KILA FOMU. FEDHA ZA FOMU ZIKISHALIPWA HAZITAREJESHA.

MALIPO YATAKUWA KWA AWAMU **TATU (3)**, NA MTEJA ATATAKIWA KUFANYA MALIPO YA ASILIMIA **HAMSINI (50%)** KWA AWAMU YA KWANZA, AWAMU YA PILI ASILIMIA **THELATHINI (30%)** NA AWAMU YA TATU ASILIMIA **ISHIRINI (20%)**. **MALIPO HAYA NI PAMOJA NA GHARAMA ZA HATI MILIKI.**

MWOMBAJI AKISHACHUKUA FOMU YA MAOMBI ATATAKIWA KUIREJESHA NDANI YA SIKU **SABA (7)** NA KWAMBA MALIPO YOTE YA KIWANJA Yawe YAMEKAMILIKA NDANI YA SIKU **TISINI (90)** BAADA YA KURUDISHA FOMU YA MAOMBI.

KWA MAELEZO NA UFAFANUZI ZAIDI FIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA- IDARA YA ARDHI AMA PIGA SIMU NAMBA **0755 986 038** NA **0715 330 616**.

TANGAZO LIMETOLEWA NA:


Simon Berge
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA**